

# CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango Fedha na Utawala)

## MAWASILIANO YA NDANI

**KWA:** Watumishi wote

**KUTOKA:** Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala)

**TAREHE:** 31.05.2023

**YAH: KUWASILISHA TAARIFA ZA UTENDAJI KAZI (OPRAS) KWA MWAKA 2022/2023 NA KUJIANDAA NA UJAZAJI WA MALENGO MAPYA YA MWAKA 2023/2024**

Itakumbukwa kwamba moja ya takwa la Kanuni za Utumishi wa Umma (2022) ni kila mtumishi wa umma kujaza na kuwasilisha taarifa za utendaji kazi (OPRAS) kwa kiongozi wake kila ifikapo au kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha yaani **Juni** ya kila mwaka, kwa msingi huo nawakumbusha watumishi wote pamoja na watendaji kutekeleza takwa hilo la kikanuni kwa kujaza na kuwasilisha tathmini za utendaji kazi kwa mwaka wa fedha **2022/2023**.

Itakumbukwa kwamba kwa mwaka wa fedha **2022/2023** ujazaji wa tathmini za utendaji kazi ulifanyika kwa njia ya nakala ngumu (hard copy) kwa mtiririko ufuatao.

- Julai 2022** watumishi walitakiwa kujaza nakala ngumu ya malengo ya utendaji kazi na kusainiwa na wakuu wao wa kazi (immediate supervisors) kisha kuziwasilisha ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango Fedha na Utawala).
- Disemba 2022**, watumishi walitakiwa kujaza na kuwasilisha "mid-year review"
- Juni 2023** watumishi wanatakiwa kujaza tathmini ya utendaji kazi wa malengo yaliyowekwa kwa mwaka **2022/23**.

Kwa maelezo hayo kila mtumishi anakumbushwa kuhitimisha kujaza fomu ya tathmini ya utendaji kazi na kuiwasilisha kwa kiongozi wake kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya mwaka ya utendaji kazi. Baada ya kukamilika kwa zoezi hilo fomu zitawasilishwa kwa wakuu wa

vitivo/kurugenzi/vitengo/vituo vya mkoa ili viongozi hawa waziwasilishe fomu hizo kwenye ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala) kabla au ifikapo tarehe **30.06.2023**. **Hakutakuwa na nyongeza ya muda kwa wale watakaochelewa kuwasilisha fomu zao.**

leleweke kwamba kutotekeleza agizo hili ni kinyume cha Kanuni za Utumishi wa Umma (2022) pamoja na Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma (Standing Orders, 2009) Pia ni kinyume na kifungu cha 14 cha Sera ya Usimamizi wa Rasilimali watu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Human Resource Management Policy and Operational Procedures, 2019).

Wakuu wa vitivo/kurugenzi/vituo na Vitengo mnakumbushwa kusimamia zoezi hili ili lifanyike kwa ufanisi na kwa wakati. Wakati huo huo tunashauri kuanza maandalizi ya kuweka malengo mapya kwa mwaka 2023/2024 ambayo yatakuwa ndani ya mpango mkakati wa chuo (OUT-RSP).

Ninashukuru kwa ushirikiano wenu,



**Francis Badundwa**

**K.N.Y: Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala)**